

# Zana ya Tathmini ya Ardhi Mwongozo wa Mtumiaji

Landesa Rural Development Institute

UKaid from the British people

Department for International Development

# YALIYOMO


Lini & Jinsi gani kampuni inapaswa kuitumia zana ya tathmini ya ardhi? ..... 4

Jinsi ya kuitekeleza Zana ya Uhakiki wa Ardhi ..... 5

Nani Anapaswa Kutekeleza Zana ya Tathmini ya Ardhi? ..... 5

Vijenzi vya orodha ya uhakiki ..... 7

Maswali ..... 7

Hali ..... 7

Maoni & uhifadhi wa nyaraka ..... 9

Vihatarishi ..... 10

Ripoti ..... 11

Hatua za ufatiliaji ..... 11

Uwezo – Ni nani atakayefanya shughuli za mpango kazi? ..... 12

Ratiba/mpango kazi ..... 13

Zana ya tathmini ya ardhi ni tathmini ya vihatarishi na mfumo wa usimamizi. Zana hii inatoa seti ya orodha ya uhakiki iliyo rahisi na inayoeleweka na ambayo inazalisha ripoti ili kuyasaidia makampuni katika kutathmini na kusimamia namna yanavyofanya kazi ya kuheshimu haki za ardhi. Zana hii inaziba pengo lililopo baina ya ahadi za makampuni za kutambua haki za ardhi na uwezo wake katika kutekeleza na kusimamia ahadi hizo katika uendeshaji wa shughuli zao.

Katika miaka ya hivi karibuni, makampuni mengi yameweka ahadi kwa ajili ya kutambua vema na kuheshimu haki za ardhi katika kipindi chote cha mchakato wa shughuli za ugavi wao. Ingawa kuweka ahadi hizo ni hatua ya kwanza madhubuti katika kufikia mafanikio makubwa ya uwekezaji wajibifu, makampuni mengi yanajitahidi kuona ni kwa namna gani yanaweza kutekeleza ahadi hizo kwa vitendo- kunzia kwenye kutokuelewa ni maswali gani yanayopaswa kuulizwa ili kupima kukubaliana na utendaji sadifu hadi kwenye kutokujua ni msaada gani wa ndani na nje unaohitajika ili kuhakikisha kampuni ina uwezo wa kutekeleza ahadi zake.

Zana ya tathmini ya ardhi imetengenezwa ili kusaidia kujenga uwezo wa makampuni kwa kuweka mfumo uliowazi na rahisi wa kufuatilia na kusimamia safari yao kuelekea kwenye utambuzi bora na kuheshimu haki za ardhi za wakulima wadogo na jamii. Kwa ufadhili kutoka Idara ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa, Landesa iliweza kutengeneza zana ya tathmini ya ardhi kulingana na Mkataba mpya wa Usalama wa Chakula na Mfumo wa Uchunguzi wa Chakula kwa ajili ya Uwekezaji wa Ardhi katika Kilimo cha Afrika. Zana hiyo imepanua wigo wa kufikiwa na Mfumo wa Uchunguzi na hutumika katika shughuli zote mpya na zilizopo, pamoja na mifano mbalimbali ya biashara (kama vile, umiliki wa mali kubwa isiyohamishika, kilimo cha mkataba). Landesa alifanya kazi kwa karibu na Illovo Sugar Africa kwa kuzipima zana hizo katika shughuli za Illovo nchini Malawi, Msumbiji na Tanzania na kisha kuziboresha zana hizo kwa kuzingatia maoni yaliyopatikana kutoka kwa wafanyakazi wa kampuni, mashirika ya kiraia, na watendaji wenye weledi.

## Lini & Jinsi gani kampuni inapaswa kuitumia zana ya tathmini ya ardhi?

Zana ya tathmini ya ardhi itayasaidia makampuni yaweze kushughulikia ufanisi wa haki za ardhi na kufanya ufuatiliaji ili kuunga mkono maridhiano ya kanuni za uwekezaji wajibifu wa ardhi. Zana hii inapaswa kutekelezwa katika mambo kadhaa ili kusaidia maendeleo ya kampuni katika kufikia uboreshaji wa utambuzi wake na kuheshima haki za ardhi za wakulima wadogo na jamii.

Kwanza, zana hii inapaswa kutumiwa kama tathmini ya msingi ili kuisaidia kampuni kuelewa vizuri masuala yanayohusiana na ardhi ambayo inakabiliana nayo, kuendeleza na kuingiza mpango wa kushughulikia masuala kama hayo kupitia sera na michakato yake. Kwa sababu makampuni mengi huanza kuzitumia sera za ardhi baada ya kuendesha shughuli zake kwa kipindi cha miaka au hata miongo, tathmini hii itahusisha umiliki wa ardhi uliopo, mchakato wa ugavi, na upatikanaji wa ardhi uliopita, pamoja na upatikanaji wowote wa ardhi unaotegemewa au upanuzi wa mchakato wa ugavi.

Tathmini hii ya kwanza na ripoti ya matokeo yake itaweka mfumo kwa ajili ya kuunganisha michakato na vitendo faafu katika mipango ya usimamizi na shughuli za kila siku za uendeshaji wa kampuni. Zana hii inapaswa kusimamiwa upya kila baada ya kipindi fulani ili kuhakikisha kuwa michakato hii inafanya kazi vizuri na inatekelezwa kwa ufanisi.

Hatimaye, zana ya tathmini ya ardhi inapaswa kutekelezwa upya mapema kabla ya kufanya upanuzi wowote wa mchakato wa ugavi au upatikanaji wa ardhi uliyopendekezwa au mabadiliko makubwa ya matumizi ya ardhi.

## Jinsi ya kuitekeleza Zana ya Uhakiki wa Ardhi

Kujenga uwezo lazima iwe ni sehemu ya msingi ya jitihada za kampuni katika kufanikisha vema uwekezaji wajibifu wa ardhi. Makampuni mengi ambayo yametoa ahadi za haki za ardhi yana uzoefu mdogo au hayana kabisa uzoefu katika kutekeleza sera zinazohusiana na ardhi au kushughulika na masuala ya ardhi katika utaratibu unaofaa na mchakato wao wa ugavi. Kwa hiyo, uongozi wa kampuni na wafanyakazi huwa hawana uelewa mkubwa juu ya ni kwa nini sera kama hizo ni muhimu au ina maana gani kuzingatia sera hizo.

Ili kushughulikia pengo hili juu ya uwezo unaohusiana na ardhi, makampuni yanapaswa kwanza kuufahamu uongozi na wafanyakazi wake, viwango vya kimataifa vilivyopo na utendaji sadifu kwa ajili ya uwekezaji wajibifu wa ardhi pamoja na athari mbaya zinazoweza kujitokeza ambazo sera hizo zinajaribu kuziepuka au kuzipunguza. Mafunzo haya yatahakikisha kwamba, wafanyakazi wanaelewa lengo na umuhimu wa sera za ardhi na umuhimu wa shughuli zinazohitajika katika utekelezaji wa sera hizo (kama vile, tathmini ya athari, ushirikishwaji wa jamii na mashauriano, nk). Kwa kufahamu ni shughuli gani zinazotakiwa kutekelezwa, makampuni pia yataweza kutambua ni ujuzi gani unaohitajika ili kukamilisha shughuli hizo, pamoja na ni nani anayefaa zaidi kutekeleza shughuli hizo. Suala hili linaweza kufanyika kuanzia kwa wafanyakazi wa kampuni hadi wadau wa nje (kama vile, AZAKi, serikali, watendaji, nk).

## Nani Anapaswa Kutekeleza Zana ya Tathmini ya Ardhi?

Wakati wajibu wa kusimamia ahadi ya ardhi ya kampuni inabaki kuwa ya uongozi wa juu, na shughuli za uendeshaji na sera zinaweza kuathiri wafanyakazi ndani ya idara, uwajibikaji wa moja kwa moja kwa ajili ya kutekeleza Zana ya tathmini ya ardhi lazima apewe mtu mmoja au timu. Kila kampuni ina upekee wake katika muundo wake wa uongozi, mamlaka na uwezo wa idara, pamoja na mipangilio ya wafanyakazi; Kwa mantiki hiyo, kila kampuni inaweza kupanga ardhi na zana ya tathmini ya ardhi kwa namna ya tofauti. Vipengele muhimu ambavyo kampuni inapaswa kuvitumia katika kufikia maamuzi haya ni pamoja na:

**Upatikanaji wa taarifa:** Mtekelezaji wa Zana ya tathmini ya ardhi atahitaji kupata taarifa za kina na kwa mawanda mapana kuhusu umiliki wa ardhi wa kampuni, masuala ya kisheria (ikiwa ni pamoja na mikataba ya uzalishaji, mikataba ya kukodisha, migogoro ya kisheria, na masuala mengine), mchakato wa uzalishaji, na sera za rasilimali watu, haya yakiwa ni baadhi tu. Kwa mantiki hiyo, utekelezaji wa zana ya tathmini ya ardhi wenye tija na unaozingatia wakati utahitaji kuwepo na upatikanaji wa unaojitosheleza wa taarifa za kina za kampuni.

**Mamlaka ya usimamizi na utoaji wa maamuzi:** Mtekelezaji wa zana ya tathmini ya ardhi anapaswa kuwa na mamlaka ya kutosha katika kutoa mapendekezo kwa vitendo vinavyotakiwa na majibu ya kimkakati ili kuhakikisha kuwa zana ya tathmini ya ardhi na ripoti ya matokeo yake inaunganishwa kwenye michakato na taratibu za kampuni.

Uwezo wa muhimu na wa msingi anaopaswa kuwa nao mtekelezaji au timu ya utekelezaji unajumuisha utii wa sheria na sera, taratibu za malalamiko, mahusiano ya kijamii, na mchakato wa usimamizi. Kutokana na stadi za aina mbalimbali, kampuni inapaswa kuteua mtu zaidi ya mmoja katika utekelezaji wa wajibu huo.

Kuanzisha na kuratibu michakato ya ndani, kukusanya data, na kujenga uwezo ni hatua muhimu katika kuwawezesha wafanyakazi wa kampuni kutekeleza kwa ufanisi zana hii. Hata hivyo, hakuna kampuni inayofanya kazi peke yake na kuweza kushughulikia masuala yote yanayohusiana na ardhi yaliyobainishwa kwenye uwekezaji: ili kufanikiwa, kampuni lazima ishirikiane moja kwa moja na mara kwa mara na jamii, wadau wa serikali, na mashirika ya kiraia. Kuelewa ushiriki na mashauriano kama kipengele muhimu cha kufanya biashara, na kuiingiza ipasavyo mikakati na michakato katika mifumo yake, ni jambo la muhimu.

## ☑ Vijenzi vya orodha ya uhakiki

Zana ya tathmini ya ardhi inajumuisha seti ya orodha ya uhakiki ambayo mtu anaweza kuitumia ili kupima iwapo uendeshaji wa shughuli za kampuni unafungamana na vipengele muhimu vya uwekezaji wajibifu wa ardhi. Vipengele hivyo muhimu hupatikana kuanzia kwenye hatua za kushauriana na kushirikiana na jamii zilizoathiriwa na uendeshaji ili kuhakikisha kwamba kampuni inaingia katika mikataba ya haki na usawa katika kupata au kutumia ardhi.

**Uhamisho:** Orodha tofauti za uhakiki hutolewa kwa kuzingatia iwapo kampuni inajitathmini yenyewe kuhusiana na umiliki wake ardhi (kama vile, mashamba makubwa inayomiliki moja kwa moja au yanayomilikiwa na watumiaji) au mipangilio ya kilimo cha mkataba (kama vile, ardhi iliyomilikiwa moja kwa moja au iliyokodishwa na wasambazaji wa kampuni). Orodha ya uhakiki wa milki ya ardhi imewekwa kwenye tabu ya pili; orodha ya uhakiki wa kilimo cha mkataba imewekwa kwenye tabu ya nne. Maelekezo ya kina ya orodha ya uhakiki wa milki na kilimo cha mkataba yanapatikana katika tabu namba moja na namba tatu, kwa kufuata mtiririko huo.

### MASWALI

Safu ya kwanza katika kila orodha ya uhakiki inajumuisha maswali ambayo kampuni inapaswa kuyajibu ili kutathmini iwapo imechukua hatua maalum zinazoonyesha kukubaliana na vipengele muhimu vya uwekezaji wajibifu wa ardhi. Maswali kama hayo yanajumuisha, kwa mfano, endapo kampuni imekubaliana na sera ya haki za ardhi au ikiwa inatoa fidia sahihi kwa wale ambao ilichukua au inaitumia ardhi yao.

### HALI

Badala ya kutoa jibu la "ndiyo" au "hapana" tu kwenye kila swali, katika safu ya pili yenye jina la "hali," mtumiaji anatakiwa kuonyesha kiwango cha maendeleo ambacho kampuni imekifikia kwa kuchagua moja kati ya machaguo matano yaliyofasiliwa hapa chini. Mtumiaji atabaini kuwa katika machaguo yote hakuna chaguo lenye asilimia 100%. Hitilafu hii ilifanyika kwa makusudi kwa sababu jitihada za kampuni kufanya

uwekezaji wajibifu wa ardhi na kwa ufanisi ni jitihada zinazobadilika na ni endelevu. Kwa hiyo, kukubaliana na vipengele muhimu vya uwekezaji wajibifu hakupaswi kuchukuliwa kama zoezi la mara moja. Badala yake, kampuni inapaswa kufanya tathmini ya utendaji wake mara kwa mara, kwa mwaka ili kuhakikisha maendeleo yanafikiwa.

- **< 25%** - Hali hii inaashiria kwamba kampuni imepiga hatua ndogo sana ya maendeleo au hakuna maendeleo yaliyofikiwa katika kategoria hiyo. Kwa mfano, kwa swali linalouliza endapo kampuni ilifanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (ESIA), kampuni inabainisha kuwa haijafanya tathmini ya namna hiyo.
- **26 – 50%** - Hali hii inaashiria kwamba kampuni imepiga hatua ndogo ya maendeleo katika kategoria hiyo. Kwa mfano, kwa swali linalouliza iwapo kampuni imefanya ESIA, kampuni hiyo inabainisha kuwa haijafanya tathmini hiyo, lakini ina mipango madhubuti ya kufanya tathmini moja katika muhula wa hivi karibuni.
- **51 – 75%** - Hali hii inaashiria kwamba kampuni imepiga hatua kubwa kidogo ya maendeleo katika kategoria hii**.** Kwa mfano, swali linalouliza iwapo kampuni imefanya ESIA, kampuni inabainisha kuwa imefanya ESIA; Hata hivyo, tathmini haikupima kwa kina athari za kijamii.
- **76 – 99% -** Hali hii inaashiria kwamba kampuni imepiga hatua kubwa ya maendeleo au inakaribia kukamilisha malengo yake katika kategoria hii. Kwa mfano, kwa swali linalouliza iwapo kampuni imefanya ESIA, kampuni hiyo inabainisha kuwa imekamilisha ESIA. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba upangaji huu haumaanishi kuwa hatua za baadaye katika kategoria hii hazihitajiki. Kwa mfano, ESIA inaweza kuwa na haki ya kufanyika katika siku zijazo ikiwa haki au matumizi ya ardhi ya kampuni yatabadilika.
- **N/A** - Hali hii inapaswa kutumiwa kwa uangalifu na iwapo tu kategoria hiyo ni wazi kwamba haitumiki kwenye uendeshaji wa shughuli za kampuni. Kwa mfano, kwa swali linalouliza iwapo sheria za ndani na sera zinazoongoza utaratibu wa kilimo cha mkataba zipo katika nchi ambapo kampuni inafanya kazi,

inawezekana kuweka alama ya "N / A" ikiwa sheria hizo hazipo. Chaguo hili linapaswa tu kutumika ikiwa kategoria hiyo haitumiki kwenye muktadha ambao kampuni inafanya kazi. Chaguo hili halipaswi kutumiwa ili kuepuka kujibu maswali ya kategeoria fulani.

## MAONI & UHIFADHI WA NYARAKA

Katika safu ya tatu, watumiaji wana fursa ya kutoa maoni na uhifadhi wa nyaraka kuelezea na kusaidia hali iliyochaguliwa kwenye safu ya pili. Hii inampa mtumiaji fursa ya kutoa maelezo kwa nini kampuni haijapata maendeleo makubwa kidogo au makubwa katika kategoria mahsusi ili kuongoza jitihada za kampuni katika kushughulikia vema suala hilo na kwa muda mrefu. Kwa mfano, inaweza kuwa kesi kwamba sera za haki za ardhi za kampuni hazishughulikii umuhimu wa haki za ardhi za wanawake; hata hivyo, kampuni inaweza kuwa katika mchakato wa kushauriana na mtaalam wa kijinsia ili kuingiza maudhui hayo. Katika hali hiyo, kampuni hiyo inapaswa kujumuisha maelezo yanayoelezea kwa kina mipango yake ya kujumuisha maudhui hayo na maelekezo ya kufuatilia na kusasisha zana za tathmini ya ardhi mara tu kategora hiyo itakapokamilika.

Zana hii pia inaruhusu watumiaji kuingiza viunga kwenye nyaraka ili kusaidia maendeleo yaliyofanyika kwenye kategoria fulani. Kwa mfano, iwapo kampuni inabainisha kuwa ina sera ya haki za ardhi na uwezo wa wafanyakazi wanaoweza kutekeleza sera hiyo, mtumiaji anaweza kutoa viunga kwenye nyaraka au vyanzo vingine vinavyotoa maelezo ya kina ya sera ya haki za ardhi na ambaye ana wajibu wa kutekeleza majukumu yanayohusiana na utekelezaji wake. Kwa kuingiza viunga kwenye nyaraka na vyanzo vingine, zana ya tathmini ya ardhi hutumika kama moja ya hazina ya taarifa ili kusaidia au kuelezea maendeleo ya kampuni hadi sasa. Zana ya tathmini ya ardhi inaweza kushirikishwa pamoja na wafanyakazi wa ndani ili kuhakikisha wafanyakazi muhimu wanapata taarifa za maendeleo yaliyofikiwa; zana inaweza pia kushirikishwa kwa watu wa nje na wadau muhimu ili kuonyesha kwamba kampuni inafanya kazi ili kufikia ahadi zake za haki za ardhi.

## VIHATARISHI

Katika safu ya nne, watumiaji wanaelekezwa kuweka kiwango kwenye vihatarishi kuanzia namba 1 – 3. Namba 1 ikiwa na maana ya kihatarishi cha kiwango cha chini, namba 2 ikiwa na maana ya kihatarishi cha kiwango cha kati, na namba 3 ikiwa na maana ya kihatarishi cha kiwango cha juu. Ingawa aina ya kihatarishi inaweza kutofautiana kutokana na kategoria, kihatarishi kinaweza kujumuisha mambo yafuatayo:

- Kihatarishi chenye sifa ya kampuni na leseni ya kijamii katika kuendesha shughuli zake
- Kihatarishi cha kuvuruga, na kinachosababisha kuongezeka kwa gharama ya uendeshaji au ucheleweshaji
- Kihatarishi cha madhara kwa wakulima wanawake na wanaume na usalama wa kumiliki ardhi kwa jamii
- Kihatarishi cha athari mbaya za kijamii, kimazingira, na kiuchumi kwa wakulima wanawake na wanaume na wanajamii
- Kihatarishi cha kutenganisha mitazamo ya wakulima wanawake na wanaume na wanajamii
- Kihatarishi cha mgogoro kati ya kampuni, wakulima, na wanajamii
- Kihatarishi cha madhara mengine yoyote kwa kampuni, wakulima, au jamii kinachotokana na uendeshaji

Inawezekana kwamba hali ya kila kategoria itahusiana na kihatarishi ilichopewa. Kwa mfano, kufanya maendeleo madogo sana au kutofanya maendeleo katika kategeoria fulani kunaweza kusababisha kihatarishi kwamba eneo hili la kutokukubaliana litasababisha masuala fulani hapo baadaye. Hata hivyo, hali na kihatarishi siyo lazima vihusiane. Kwa mfano, kampuni inaweza kufanya maendeleo mazuri kuelekea kwenye ubainishaji wa maeneo ya uingiliaji wa ardhi ya mtu mwingine uliofanyika zamani, wa sasa, na unaojitokeza; hata hivyo, suala la uingiliaji wa ardhi ya mtu mwingine bado linaweza kuwa lililoenea na ni endelevu. Kwa hiyo, mtumiaji angependa kutoa kiwango cha juu kabisa cha kihatarishi ili kuakisi ukweli kwamba kategoria hiyo bado inaonesha kihatarishi kwa kampuni, wakulima, na jamii, kwa hiyo, inapaswa kupewa kipaumbele.

## Ripoti

Wakati orodha ya uhakiki inaisadia kampuni kujitathmini imefikia wapi kuhusiana na ahadi zake, sehemu ya taarifa ya zana ya tathmini ya ardhi inasaidia mipango ya muda mfupi na ya kati kwa kubainisha na kuweka kipaumbele kwenye maeneo ya uboreshaji na kutoa nafasi kwa kampuni ili kupanga hatua zinazofuata.

Baada ya kukamilisha kila orodha ya uhakiki, moja kwa moja ripoti itadokeza tabu inayofuata kwenye kategoria zote zilizopewa hali ya ukamilifu wa asilimia <51% au kategoria yoyote iliyopewa kihatarishi namba 2 (kati) au namba 3 (juu). Vigezo hivi viliwekwa kama jitihada ya kuyasaidia makampuni kuweka kipaumbele kwenye maeneo ambayo wamefanya maendeleo kidogo sana, kidogo, au hakuna maendeleo yoyote, pamoja na maeneo ambayo yamedhihirisha kuwepo kwa kihatarishi kikubwa kwenye makampuni, wakulima na jamii. Safu ya kwanza mpaka ya nne moja kwa moja na kwa uzingativu itajazwa na kipengele cha orordha ya uhakiki (jina la orodha kuu ya uhakiki), hali, na kihatarishi. Kwa njia hiyo, mtumiaji atakumbushwa kuhusu hali na vihatarishi gani walivyoainisha kwenye kipengele cha orodha ya uhakiki, ambavyo vinazuia hitaji la urejerezi kwenye orodha ya uhakiki.

### HATUA ZA UFATILIAJI

Katika safu ya tano yenye jina la, "Hatua za ufuatiliaji," watumiaji wanatakiwa kuelezea hatua za ufuatiliaji ambazo kampuni itachukua ili kufikia maendeleo na kuelekea kwenye kukamilisha kipengele cha orodha ya uhakiki na kupunguza vihatarishi. Kueleza kwa kina hatua za ufuatiliaji ni jambo la muhimu ili kuhakikisha kwamba uongozi na wafanyakazi muhimu hawana uelewa wa maeneo ya kihatarishi na yasiyokubaliana na vipengele muhimu vya uwekezaji wajibifu wa ardhi, lakini pia wanachukua hatua madhubuti katika kuhakikisha wanaingia katika makubaliano na kupunguza vihatarishi hivyo ili kuweza kwenda mbele.

Kwa mfano, ikiwa ripoti inajumuisha kipengele cha orodha ya uhakiki kinachoashiria kwamba kampuni haijafanya maendeleo makubwa au muhimu katika kushauriana na wanajamii walioathiriwa na shughuli zao, kisha kampuni inaweza kuzielezea kwa kina

hatua za ufuatiliaji ili kuongeza na kuboresha mawasiliano na jamii hizo. Hatua hizo zinaweza kujumuisha, kwa mfano, kutengeneza mkakati wa mashauriano na ushirikiano ambao unajumuisha kufanya mikutano ya kila mwezi na viongozi wa jamii na wanajamii ili kuelewa vema ni kwa namna gani shughuli hizo zinaathiri jamii na endapo kuna migogoro yoyote ya ardhi isiyojulikana kati ya kampuni na jamii.

## UWEZO – NI NANI ATAKAYEFANYA SHUGHULI ZA MPANGO KAZI?

Katika safu ya sita, yenye jina "uwezo," watumiaji wataonyesha ni watendaji gani wa ndani na nje watakuwa na wajibu wa kuchukua hatua za ufuatiliaji zilizoelezewa kwa kina katika safu ya tano. Wakati wa kupima zana ya tathmini ya ardhi, suala hili liliibuliwa kwamba hata kama makampuni yanaelewa kuhusu masuala ya ardhi na ni hatua gani za kuchukua ili kuyashughulikia, mara nyingi hushindwa kubainisha ni nani atakayewajibika katika kuchukua hatua hizo. Kwa hiyo, watumiaji watatakiwa kueleza kwa kina ni watendaji gani wa ndani na wa nje (kama vile, AZAKi, watendaji wenye weledi, serikali, nk) watakuwa na wajibu wa kuchukua hatua hizo.

Ni muhimu kutambua kwamba ingawa zana ya tathmini ya ardhi ina lengo la kuyasaidia makampuni kutekeleza ahadi zao ili kutambua vizuri na kuheshimu haki za ardhi, haiwezekani kwamba, kampuni yoyote na kwa upekee wake itakuwa na stadi mbalimbali na utaalamu unaohitajika kuikabili kila hali inayoweza kujitokeza. Badala yake, huenda wakahitaji kutegemea kwenye mikakati ya ushirikiano na wadau muhimu ili kujaza mapengo yoyote ya uwezo. Kwa mfano, kampuni inaweza kubainisha mipaka isiyoeleweka kama sababu inayochangia kufikia kwenye masuala ya uingiliaji wa ardhi ya mtu mwingine na wanajamii ambao hawawezi kubainisha sehemu ilipo mipaka. Ili kushughulikia suala hilo, kampuni hiyo inaweza kumpa kazi mpima ramani wa nje ili aweze kuifatilia mipaka na kubainisha maeneo ya uingiliaji wa ardhi wakati huo pia ikaajili mtu wa mwingine, kama vile CSO au mtendaji mwenye weledi, ili aweze kushauriana na jamii inayoishi pembezoni mwa mipaka kwa kuzingatia ukweli kwamba mipaka inahitaji kuwekwa bayana na kufuatiliwa. Sambamba na hilo, ikiwa kama kampuni inahitaji kufanya ESIA ili kuelewa jinsi gani shughuli zake zilizopanuliwa

zitaathiri haki za ardhi za jamii na maisha, inaweza kuhitaji kukodisha mtaalam wa tatu ili kutoa msaada wa ziada juu ya namna ya kupima na kupunguza madhara hayo.

## RATIBA/MPANGO KAZI

Katika safu ya saba, yenye jina la "Ratiba na Mpango kazi" makampuni yanaelekezwa kutoa maelezo ya kina juu ya ratiba na mpango kazi halisi wa kukamilisha mipango ya utekelezaji iliyoainishwa kwenye safu ya "ufuatiliaji wa hatua". Ratiba na mpango kazi huo unapaswa kutumiwa katika kuwasimamia watendaji wa ndani na nje wanaowajibika kukamilisha hatua za ufuatiliaji kwa wakati muafaka. Ratiba na mpango kazi huo unapaswa kupitiwa upya mara kampuni inapoanza kuchukua hatua za ufuatiliaji ili kuhakikisha uhalisia. Kwa kuingiza muda uliopangwa wa kukamilisha hatua za ufatiliaji, zana ya tathmini ya ardhi inaweza pia kutumika katika kutoa taarifa kwa upande wa nje kuhusiana na ni lini kampuni inatarajiwa kufanya maendeleo ili kufanikisha utekelezaji wa ahadi zake za kutambua vema na kuheshimu haki za ardhi.